# KUCHUNGUZA MBINU ZA KIKORASI KATIKA TAMTHILIYA YA SADAKA YA JOHN OKELLO NA MONDLANE NA SAMORA: UTAFITI LINGANISHI

**MARYAM ALI OMAR**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNIKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu yenye mada, "**Kuchunguza Mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*: Utafiti linganishi**" na kupendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**………………………………………**

**Prof. Emmanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

**Tarehe………………………...**

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ni kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili, Utafiti na Uchapaji kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TAMKO

Mimi **Maryam Ali Omar**, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

**Saini……………………………….**

**Tarehe……………………………….**

## TABARUKU

Napenda kuitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu: Ali Omar Yussuf na Asha Hemed Salim, mume wangu, watoto wangu pamoja na ndugu zangu.

## SHUKURANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, uzima, afya, nguvu na fahamu katika kipindi chote cha masomo yangu hadi leo nimefikia ngazi hii ya elimu. Kwa udogo wa shukurani ninasema “Alhamdulillahi”.

Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa utafiti huu, Prof. Emmanuel Mbogo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Mawazo yake yalikuwa ya msingi sana hadi leo nimekamilisha tasnifu hii. Ninachoweza kusema ni kutoa ahsante kwa Prof. Emmanuel Mbogo na kumuombea Mungu ambariki kwa amjalie afya njema na maisha marefu. Amin.

Tatu, shukurani nyingi ziufikie uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kuanzia makao makuu Dar es Salaam hadi tawi la Pemba. Kwa vile hawa ni wengi naomba niwataje baadhi yao; Dkt. Muhammed Omary Maguo, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Hilda Pembe, mwalimu Bakari Kombo Bakari, mwalimu Nassor Ali Suleiman, na wengineo, Hawa wote walisaidia kwa njia moja ama nyengine hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

Nne, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu yote bila kuwasahau wazazi wangu: Ali Omar Yussuf na Asha Hemed Salim; mume wangu Saleh Mohd Said na mtoto wangu Salhiin Saleh Mohd na ndugu zangu wengine. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu na ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha masomo na utafiti huu. Nawaombea kwa Mungu awape baraka na neema zisizo mfano.

Pia, ninapenda kutoa shukrani kwa Mwalimu Hemed Said Massoud, Mwalimu Sharif Juma Fakih, Ali Mussa Faki, Muhammed Ali Salim, kwa kuwa bega kwa bega katika hatua zote muhimu za utafiti huu kuanzia mwanzo mpaka kukamilika kwake.

# IKISIRI

Utafiti huu ni linganishi ambao lengo kuu ni kuchunguza mbinu za kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*. Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* ni tamthiliya za kihistoria zilizotungwa na mtunzi maarufu wa fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania Profesa Emmanuel Mbogo. Ili kufikia malengo ya utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia ya Korasi na Fasihi Linganishi. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia njia ya maktabani. Uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu zilitumia mkabala wa kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa tamthilia teule zote zimetumia mbinu za kikorasi kama vile; korasi kama kimya, korasi kama wimbo, korasi kama mhusika, korasi kama tukio la mila na desturi, korasi kama mtindo na korasi kama muundo. Pia, utafiti umebaini kuwa mbinu za kikorasi katika tamthilia teule vimebeba dhamira kama vile; mapinduzi, ukoloni, umoja na mshikamano, ujasiri, umuhimu wa elimu, itikadi na lengo la ukombozi wa bara la Afrika. Aidha, data za utafiti huu zimeonesha kuwa tamthiliya teule zimelingana katika matumizi ya mbinu za kikorasi. Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* zote zimetumia korasi kama kimya, korasi kama mhusika, korasi kama dhamira, kama tukio la mila na desturi, korasi kama muundo na korasi kama mtindo. Kwa mfano, tamthilia ya *Mondlane na Samora* inatumia mapambano ya Frelimo dhidi ya Wareno huko Msumbiji kama tukio la mila na desturi ili kuibua dhamira za mapinduzi na ukombozi na tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* inatumia mapambano ya Wazanzibar dhidi ya utawala wa Jamshidi ili kuibua dhamira ya mapinduzi na ukoloni. Pia, utafiti huu umebaini kuwa pamoja na kufanana kwa kiwango kikubwa kwa matumizi ya korasi katika tamthiliya teule kuna baadhi ya matumizi ya korasi kama vile; korasi kama mhusika, korasi kama tukio la mila na desturi na korasi kama dhamira kuna aina fulani ya tafauti. Kwa mfano, korasi kama tukio la mila na desturi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* linajitokeza katika kukabidhiwa madaraka Jemshidi kutoka kwa Waingereza na katika mapinduzi ya Zanzibar. Kwa upande wa tamthiliya ya Mondlane na Samora korasi kama tukio la mila na desturi inajitokeza kupitia kifo cha Mondlane, safari ya Nyerere alipokwenda Msumbiji, sherehe ya harusi ya Samora na Josina, vita katika msitu wa Msumbiji vilivyoongozwa na wapambanaji wa Frelimo na mkutano wa kusherehekea uhuru kutoka kwa Wareno

## YALIYOMO

UTHIBITISHO.......................................................................................... ii
HAKIMILIKI ......................................................................................... iii
TAMKO……… ......................................................................................iv
TABARUKU..........................................................................................v
SHUKURANI ........................................................................................vi
IKISIRI……......................................................................................... viii
YALIYOMO ..........................................................................................ix
ORODHA YA MAJADWELI ................................................................xiv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ..........................................1**
1.1 Utangulizi.........................................................................................1
1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti.................................................................1
1.3 Tatizo la Utafiti ................................................................................4
1.4 Malengo la Utafiti ............................................................................6
1.4.1 Lengo kuu .....................................................................................6
1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti ..........................................................6
1.5 Maswali ya Utafiti.............................................................................6
1.6 Umuhimu wa Utafiti..........................................................................7
1.7 Mipaka ya Utafiti ..............................................................................8
1.8 Muundo wa Tasnifu...........................................................................9
1.9 Hitimisho .........................................................................................10

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA............................................................11**

2.1 Utangulizi..........................................................................11
2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi ..................................................11
2.3 Dhana ya Korasi..................................................................14
2.3.1 Aina za Korasi..................................................................17
2.3.1.1 Korasi kama Mhusika......................................................18
2.3.1.2 Korasi kama Tukio la Mila na Desturi ..............................19
2.3.1.3 Korasi kama Mtindo........................................................19
2.3.1.4 Korasi kama Dhamira......................................................20
2.3.1.5 Korasi kama Wimbo........................................................21
2.3.1.6 Korasi kama Muundo ......................................................22
2.3.1.7 Korasi kama Kimya.........................................................22
2.4 Utafiti linganishi katika Tamthiliya ya Kiswahili..................24
2.5 Tafiti Kuhusu Korasi Katika Kazi Mbalimbali......................27
2.6 Pengo la Utafiti ..................................................................30
2.7 Mkabala wa Nadharia..........................................................30
2.7.1 Nadharia ya Fasihi Linganishi ..........................................31
2.7.2 Nadharia ya Korasi...........................................................33
2.7.2.1 Misingi ya Nadharia ya Korasi ........................................34
2.7.2.2 Aina za Korasi katika Mtazamo wa Kisasa .......................35
2.8 Hitimisho ............................................................................35

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI..........................................................36**
3.1 Utangulizi..........................................................................................36
3.2 Umbo la Utafiti ....................................................................................36
3.3 Eneo la Utafiti .....................................................................................37
3.4 Kundi Lengwa......................................................................................37
3.5 Sampuli ...............................................................................................37
3.6 Usampulishaji.......................................................................................38
3.6.1 Usampulishaji Lengwa .......................................................................38
3.7 Data za Utafiti Zilizokusanywa............................................................39
3.7.1 Data za Msingi ...................................................................................39
3.7.2 Data za Upili ......................................................................................40
3.8 Mbinu za Kukusanya Data...................................................................41
3.8.1 Usomaji Makini...................................................................................41
3.8.2 Upitiaji wa Nyaraka.............................................................................42
3.9 Mkabala wa Uchambuzi wa Data za Utafiti ..........................................42
3.10 Zana za Kukusanyia Data ...................................................................43
3.10.1 Shajara .............................................................................................43
3.10.2 Kompyuta..........................................................................................43
3.11 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti.............................................43
3.11.1 Usahihi wa Data ...............................................................................43
3.11.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti...........................................................44
3.11.3 Maadili ya Utafiti ..............................................................................44
3.12 Hitimisho ...........................................................................................45

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ..................46**

4.1 Utangulizi..............................................................................................46

4.2 Usuli wa Mwandishi Emmanuel Mbogo ..............................................46

4.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* .............................49

4.4 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ...............................50

4.5 Matumizi ya Mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na Mondlane na Samora..................................................51

4.5.1 Matumizi ya Mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ...........................................................................................52

4.5.1.1 Korasi kama Kimya.................................................................................52

4.5.1.2 Korasi kama Wimbo................................................................................55

4.5.1.3 Korasi kama Dhamira..............................................................................57

4.5.1.4 Korasi kama Mila na Desturi ..................................................................59

4.5.1.6 Korasi kama Muundo .............................................................................69

4.5.1.7 Korasi kama Mtindo................................................................................70

4.5.2 Matumizi ya Mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora ...........................................................................................72

4.5.2.1 Korasi kama Kimya.................................................................................72

4.5.2.7 Korasi kama Mtindo................................................................................86

4.5.3 Mbinu za Kikorasi zilivyoibua Dhamira katika Tamthiliya teule...........88

4.5.3.1 Mbinu za Kikorasi Zilivyoibua Dhamira katika *Sadaka ya John Okello* ...........................................................................................88

4.5.3.2 Mbinu za vya Kikorasi zilivyoibua Dhamira katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora.............................................................111

4.5.4 Ulinganishaji na Utofautishaji wa Mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello na Mondalane na Samora.........133
4.5.4.1 Kulinganisha Mbinu za Kikorasi na Dhamira katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John* Okello na Mondlane na Samora...............................134
4.5.4.2 Kutofautiana kwa Mbinu za Kikorasi na Dhamira katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*............................139
4.6 Hitimisho ..........................................................................143

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........144**
5.1 Utangulizi.........................................................................144
5.2 Muhtasari .........................................................................144
5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza ..............................................146
5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili........................................................147
5.2.3 Lengo Mahsusi la Tatu ......................................................147
5.3 Hitimisho ..........................................................................149
5.4 Mapendekezo .....................................................................149
5.4.1 Kwa Watafiti Wengine .......................................................149
5.4.2 Kwa serikali ......................................................................150
5.4.3 Mapendekezo kwa jamii....................................................150

**MAREJELEO……… .........................................................................151**

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli 01: Muhtasari wa Mbinu za Kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ....71

Jadweli 02: Muhtasari wa Mbinu za Kikorasi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*....87

Jadweli 03: Muhtasari wa jumla wa Mbinu za Kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*....87

Jadweli 04: Muhtasari wa Ulinganishaji wa jumla wa mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello na Mondlane na Samora ....141

Jadweli 05: Muhtasari wa jumla wa tofauti ya dhamira zilizoibuliwa na mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* ....142

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Bi | Bibi |
| Bw. | Bwana. |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar. |
| Dkt | Daktari. |
| M.A | Master of Art. |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. |
| OUT | Open University of Tanzania. |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Mada ya utafiti huu imehusu: Kuchunguza mbinu za kikorasi katika tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*: Utafiti Linganishi. Sura hii ni sura tangulizi inayobainisha vipengele mbalimbali vya msingi vinavyohusu utafiti huu. Vipengele vilivyoainishwa ni pamoja na mada ya utafiti, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti ambayo utafiti huu unakusudia kuyajibu, umuhimu, mipaka ya utafiti, muundo wa utafiti na hitimisho.

## 1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Korasi imeelezwa kuwa ni dhana iliyokuwa ikitumiwa na Wayunani wa kale katika shughuli zao za matambiko ya kijadi ambayo walikuwa wakiyafanya.Katika kuielezea dhana hii Smpson na Weiner (1979:38) kama wanavyonukuliwa na Mutembei (2012:8) wanaielezea korasi kuwa ni kikundi cha waimbaji na wachezaji katika sherehe za kidini na sanaa za maonyesho za Uyunani ya kale. Huu ulikuwa ni mtazamo wa kijadi kuhusu dhana ya korasi na jinsi ilivyokuwa ikitazamwa kihistoria katika jamii ya Wayunani. Hata hivyo ni dhahiri kwamba maana hii ya korasi ina ufinyu fulani kwani korasi katika mkabala wa kifasihi ni zaidi ya kikundi cha waimbaji na wachezaji katika sherehe za kidini na sanaa za maonesho. Kwa sasa korasi inajitokeza katika kazi za fasihi kama vile riwaya na hata ushairi. Mtazamo huo ndio uliosababisha wataalamu na watafiti mbali mbali kuanza kuitazama dhana ya korasi kwa jicho la ndani zaidi. Kwa mfano, Webster (1961:471) wanaeleza kuwa korasi ni kikundi cha waimbaji au waongeaji. Dhima ya awali iliyokuweko katika

Uyunani ya kale sasa ilianza kubadilika. Kwa hali hiyo, wanaeleza kuwa dhima ya korasi sasa ilikuwa ni ile ya wahusika katika kitendo na wafasiri wa kitendo.

Aidha, Webster (1986) wanafafanua dhana ya korasi kwa kulilinganisha neno hili na neno la "Kilithunia" lenye maana ya "kisababishi" wanaeleza kuwa neno "zaras" inayokaribiana kimaana na neno korasi ni dhana inayofafanua hali ya kusababisha jambo au kulifanya litokee. Chimbuko kubwa la korasi ni uimbaji na maongezi kama sehemu muhimu ya ujenzi wa korasi. Kwa hali hiyo ni vyema tugusie swala la utamaduni ambalo linaingizwa katika kipengele cha dhana ya korasi. ambalo limegusiwa linalohusu dhana ya korasi, suala hilo ni suala la kiutamaduni la utambaji (Mutembei, 2012:8-9).

Saidensticke (2005) anaeleza kuwa shughuli ya tambiko iliyojuilikana kama "dithirambu" watambaji walijitokeza huku wakiimba kwa sauti moja huku wakiongozwa na uimbaji wa kikorasi. Shuguli hii ya utambikaji ilihusu jamii nzima na ikawa ni desturi ya ufanyaji matambiko yaliyomhusu kila mtu. Hivyo kila mtu akawa ni sehemu ya korasi na akihusika katika kuimba na akishiriki kuwa sehemu ya jamii kwenye tambiko kwa mungu wao "Dionizi". Saidensticke (kashatajwa) anazidi kutufafanulia jinsi ilivyochukuliwa dhana hii ya korasi katika jamii za kale na hivyo ni dhahiri kuwa matukio yaliyotajwa ambayo ni matukio ya kijamii ndio yaliyochorwa kama ni korasi tu, jambo ambalo kwa sasa wazo hili linachukuliwa kama ni sehemu moja tu ya korasi.

Mutembei (2012) anaeleza kuwa dhana ya korasi inapasa kuangaliwa katika mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni kuiangalia korasi `kidayakronia` na

mkabala wa pili ni kuiangalia korasi `kietimolojia`. Mutembei (ameshatajwa) anaieleza kwamba dhana ya korasi iliibuka katika uimbaji wa kimatambiko kwa upande mmoja na ilijidhihirisha katika usanii wa Kiyunani ambao huenda sambamba na mchango wa `Aeschylos` ambaye aliigiza katika sanaa za maonesho na hasa katika drama za kitanzia. Kihistoria korasi ilikuwepo hata kabla ya michezo ya kuigiza ambayo ilitokana nayo na kwa hakika korasi ilitakiwa iwe kama ilivyokuwa mwanzoni; yaani kundi lililoteuliwa kuisema jamii nzima (Brown, 1969:56).

Kihistoria katika fasihi ya Kiswahili korasi ni nadharia mpya ya uhakiki wa fasihi katika fasihi ya Kiswahili ambapo kwa muda mkubwa wahakiki wengi waliichukulia maana ya korasi kwa ufinyu mkubwa. Kwa mfano, Masoko na Mdee (1984:53) walieleza kuwa korasi ni kiitikio. Tuonavyo ni kwamba maana hii ilikuwa ni finyu sana kwani kiitikio ni kipengele kimoja tu cha korasi ambacho kipengele hicho hujitokeza zaidi katika ushairi.

Senkoro (1988:90) kama alivyonukuliwa na Mutembei (2012:6) ameiita korasi kuwa ni mkarara. Maana hii pia imejikita katika utanzu wa ushairi ambao utanzu huu hujumuisha tenzi, mashairi na nyimbo ambapo mkarara umechukuliwa kwa dhana ya kukariri au kurudia rudia. Maana hii iliyotolewa na Senkoro (khj), inayohusu dhana ya korasi, tunakubaliana na mawazo ya Mutembei (khj) kuwa dhana hiyo ina maana finyu kwani imejikita zaidi katika fani na kuitenga kabisa maudhui. Mutembei (khj), anaeleza, lengo kuu la korasi ni kusaidia waigizaji au watazamaji kuwa na hamasa na hamu zaidi ya kazi yao hadi mwisho wa tamthiliya au igizo. Hivyo baada ya kudurusu mawazo mbali mbali ya wataalamu juu ya dhana ya korasi, katika kazi hii tumeegemea mkabala wa mawazo ya Mutembei ambapo anaiona korasi kama ni

matendo, fikra au maneno ya kisanaa ayatendayo mtu mmoja au zaidi katika kazi ya kifasihi au kuhusiana na kazi hiyo ya kifasihi ambapo hadhira hushirikishwa au huifanya hadhira au msomaji wa kazi ya fasihi alitafakuri juu ya undani wa kitendo au maelezo hayo. Maneno hayo yanaweza kuwa ya kinudhumu au kinathari. Aidha, matendo hayo yaweza kuambatana na maneno au bila ya matumizi ya maneno.

Tamthiliya ya Kiswahili kama ilivyo tamthiliya nyengine ulimwenguni imekuwa ikitumia mtindo wa korasi katika kusaniiwa. Miongoni mwa tamthiliya zilizotumia mbinu hii ya korasi ni tamthiliya ya *Sadka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* zilizoandikwa na E. Mbogo. Tamthiliya hizo zimechota mbinu hiyo katika kuibua dhamira za mtunzi alizozikusudia. Hata hivyo ilionekana kuwa bado hazijatafitiwa ili kuchunguza mtindo huo wa korasi.

Kutokana na mjadala huo wa dhana ya korasi, mtafiti aliona kuna haja ya kufanya utafiti ili kuona ni namna gani watunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili huitumia mbinu ya korasi katika kusanii kazi hizo. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza matumizi ya korasi katika tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anafumbata mbinu ya korasi katika kazi zake za sanaa.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Dhana ya korasi ilitazamwa na Wayunani kwa miktadha ya shughuli zao za matambiko ya kijadi ambayo walikuwa wakiyafanya. Katika kuielezea dhana hii ya korasi Sampson na Weiner (1979:384), kama wanavyonukuliwa na Mutembei (2012:8) wanaielezea korasi kuwa ni kikundi cha waimbaji na wachezaji katika

sherehe za kidini na sanaa za maonyesho za Uyunani ya kale. Mutembei (2012) anaona kwamba dhana hii leo imetanuka na kuwa zaidi ya kikundi cha watu wenye kuimba kwa pamoja. Hadi sasa watafiti kadhaa wamewahi kufanya utafiti kuhusu dhana ya korasi. Weiner (1979:384), Wikipedia (2010), Mutembei (2012), Salim (2015), na Hishon (2016), ni miongoni mwa watafiti hao. Mathalani Mutembei (2012), alifanya uchunguzi wa korasi na kugundua kuwa katika miktadha ya kifasihi korasi huweza kuwa katika matapo saba ambayo ni korasi kama mhusika, korasi kama kimya, korasi kama wimbo, korasi kama tukio la mila na desturi, korasi kama dhamira, korasi kama muundo na korasi kama mtindo.

Naye Hishon (2016) anasema kuwa lengo la korasi katika jamii ya Wayunani wa kale ilikuwa ni kutoa utangulizi na ufupisho kwa hadhira kuhusu kile kinachozungumziwa katika kazi ya fasihi. Ukweli ni kwamba tumetalii machapisho kadhaa hatukuona kazi iliyokwisha kutafiti matumizi ya vipengele vya korasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* kwa mkabala wa Fasihi linganishi. Hii ni kusema kuwa suala la korasi halijaguswa na watafiti wengine katika tamthiliya teule. Hivyo basi, Swali linalotatiza utafiti huu ni Je, ni mbinu zipi za korasi zimetumika katika tamthiliya za Kiswahili? Je, vipengele vya korasi vimebeba dhamira gani katika tamthiliya teule? Kutokana na maswali hayo, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mbinu za kikorasi zinavyojitokeza katika tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* ili kubaini jinsi mtunzi wa tamthiliya hizo alivyotumia mbinu hizo kama mbinu ya kisanaa katika tamthiliya za Kiswahili.

## 1.4 Malengo la Utafiti

Utafiti huu umegawanywa katika malengo ya aina mbili: Lengo kuu na malengo mahsusi kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo kuu

Kutathmini mbinu za kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane* na *Samora* kwa mkabala wa kiulanginishi.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

i. Kubainisha mbinu za kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora.*

ii. Kubainisha dhamira zilizoibuliwa na mbinu za kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello na Mondlane na Samora.*

iii. Kulinganisha na kutofautisha mbinu za kikorasi na dhamira katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i. Ni mbinu zipi za kikorasi zinazopatikana katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora?*

ii. Ni dhamira gani zilizoibuliwa na mbinu za kikorasi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora?*

iii. Ni mbinu zipi za kikorasi na dhamira zilizolingana na kutofautiana katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora?*

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti ni kazi ya kitaaluma ambayo huwa na umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya mtafiti, jamii, kitaifa na kimataifa. Utafiti huu una umuhimu katika maeneo ya msingi ya kitaaluma, kinadharia, kisera na kwa mtafiti kama ifuatavyo:

**Kitaaluma:** Matokeo ya utafiti huu yatakuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wanafunzi, walimu na wasomi wengine wa kazi za fasihi watayatumia matokeo ya utafiti huu kuwa sehemu ya marejeo yao ya kukamilisha malengo na madhumuni ya utafiti wao watakaokuwa wanaufanya. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatatumika kama sehemu ya kujiimarisha, ili kubainisha pengo la maarifa ambalo wao watalijaza katika utafiti wao. Wanataaluma ambao ni walimu, wahadhiri na maprofesa katika taaluma ya fasihi wataitumia kazi hii kama marejeleo yatakayosaidia katika kuandika vitabu, makala na maandalio ya masomo ya kufundishia wanafunzi wao wa ngazi tafauti za elimu.

**Kinadharia:** Utafifiti huu utatoa uthibitisho kwamba, nadharia za uhakiki wa fasihi zinapotumika kuhakiki kazi za fasihi huifanya kazi hiyo kuwa imara na yenye mashiko ambayo huaminika kitaaluma. Kupitia utafiti huu watafiti wa baadaye wataona umuhimu wa kutumia nadharia ya korasi katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Hivyo, nadharia hii itajidhihirisha katika kazi hii kivitendo, jambo ambalo litatoa dira na mwongozo katika uchambuzi wa kazi za fasihi hasa katika uwanja wa kutathmini matumizi ya korasi na dhamira kwa mkabala wa kiulinganishi.

**Kisera:** Utafiti huu utaeleza dhamira zinazoonesha matatizo mengi ya kijamii ambayo yanaikumba jamii kwa sasa kama vile, masuala ya elimu, ukoloni

mamboleo, usaliti, matabaka na umasikini kwa kadri matatizo hayo yalivyojadiliwa katika kazi za mwandishi teule. Kwa watunga sera, utafiti huu utawafaa katika kuainisha mambo ambayo yanastahili kuingizwa katika sera na kufanyiwa utekelezaji ili kuimarisha mipango ya utekelezaji kwa manufaa ya ujenzi wa jamii mpya endelevu.

**Kwa Mtafiti:** Utafiti huu utakuwa na manufaa kwa mtafiti kwa sababu utajibu maswali ambayo alikusudia kuyabaini. Kukamilika kwa utafiti huu kumewezesha mtafiti kupata uwelewa wa kina kuhusu dhana ya korasi na namna Emmanuel Mbogo anavyoitumia korasi kama mbinu ya kusanii tamthilia zake ili kuibua dhamira alizozikusudia kwa jamii.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Japokuwa mwandishi teule ameandika kazi nyingi za fasihi kama vile; *Watoto Wetu* (1972), *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Morani* (1993), *Fumo Liyongo* (2009), *Sundiata* (2011), *Sadaka ya John Okello* (2014) *na Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Wangari Maathai (2015), Mondllane na Samora* (2016), *Mtumwa hadi Siti binti Saad* (2018). Pamoja na tamthiliya hizo, ametunga pia riwaya kama vile; *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Vipuli vya Figo* (2008), na *Siri ya Maisha* (2010). Katika utafiti huu tulichagua tamthiliya zake mbili za *Sadaka ya John Okello na Mondlane* na *Samora* ili kuziwakilisha tamthiliya nyengine zilizoandikwa na mwandishi huyu. Hii ni kusema kuwa kiini cha mjadala wetu kilikuwa kimejikita katika tamthiliya hizo mbili teule katika kutathmini matumizi ya karosi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* kwa mkabala wa Fasihi Linganishi. Pia, data zilichambuliwa

kwa njia ya maelezo na takwimu. Emmanuel Mbogo ana tamthiliya nyingi hata hivyo kazi hii ilijikita kuchunguza matumizi ya korasi katika tamthilia ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* tu, hii ni kwa sababu isingekuwa rahisi kufanya uchunguzi wa tamthiliya zote za mwandishi huyu kwa wakati mmoja.

### 1.8 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza Mbinu za Kikorasi katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello na Mondlane na Samora: Utafiti Linganishi* una sura kuu tano (5) zifuatazo:

**Sura ya Kwanza** – Utangulizi wa Jumla: Sura hii imehusu vipengele muhimu vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, muundo wa tasnifu na hitimisho.

**Sura ya Pili** – Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia: Sura hii imelenga vipengele vifuatavyo: Utangulizi, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia: Nadharia ya Korasi na nadharia ya Fasihi Linganishi na hitimisho.

**Sura ya Tatu** – Mbinu za Utafiti: Sura hii imewasilisha vipengele vifuatavyo: Utangulizi, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data, kuaminika, kuthibitika kwa data na miiko ya utafiti na hitimisho.

**Sura ya Nne** – Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data za Utafiti: Sura hii ina sehemu ndogo ndogo zifuatazo: Utangulizi, usuli wa mwandishi Emmanuel Mbogo, muhtasari wa tamthilia ya*Mondlane na Samora* na *Sadaka ya John Okello*, vipengele

vya korasi vilivyotumika katika tamthilia teule, namna vipengele vya korasi vinavyoibua dhamira za mtunzi katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*

**Sura ya Tano** – Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo. Sura hii imeeleza vipengele vya msingi vifuatavyo: Muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti huu kutegemea maswali ya utafiti. Vile vile sura hii imetoa hitimisho na mapendekezo.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imeonesha uwasilishaji wa vipengele vya kiutangulizi vilivyotoa picha kamili ya kile kilichotafitiwa. Hili linathibitika kupitia vipengele vya mada ya utafiti, usuli wa mada ya utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vyengine ni umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Katika sura hii tumeonesha malengo ya utafiti huu na namna malengo hayo yalivyoongozwa na maswali ya utafiti ambayo yalijibiwa katika sura ya tano ya tasnifu hii.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mapitio ya maandiko tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni mapitio ya tafiti za tamthiliya zilizotangulia na dhana ya korasi na sehemu ya pili ni kiunzi cha nadharia.

## 2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi

Utafiti huu ni utafiti linganishi, hivyo kuieleza dhana ya Fasihi Linganishi imeonekana kuwa na umuhimu mkubwa sana ili kutoa uelewa wa dhana hiyo kwa ujumla. Dhana ya kulinganisha fasihi za jamii mbalimbali au mataifa mbalimbali ilianza zama za kale zaidi. Wakati huo jamii zilikuwa zinaongozwa na misingi mahususi katika kulinganisha utendekaji wa fasihi zao na za jamii nyingine. Misingi hiyo ilitokana na jamii zilizokuwa na nguvu ya kihadhi (Ponera, 2014). Kwa mfano, wakati wa mwanafalsafa wa Kiyunani Aristotle, zilishuhudia kuwepo kwa ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi mbalimbali za tamthiliya kwa lengo la kuchuja na kupata kazi bora zilizoafikiwa kupelekwa kwa hadhira. Halikadhalika zama za baada ya Kristo zilijihusisha na ulinganuzi wa matini za kidini (Biblia), wakati ambapo wasanii wa Kiarabu wa enzi za kati walijihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi za sanaa.

Kihistoria Ponera (2014) anasema kwamba katika umbo la sasa la kitaaluma, dhana ya Fasihi Linganishi ilianza huko Ufaransa mwishoni mwa karne ya 19 na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya ishirini (20), ikijikita zaidi katika utanzu wa

tamthiliya kwa sababu utanzu wa riwaya ulikuwa bado mchanga. Maarifa ya awali ya taaluma hii yalijikita katika kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na mambo yamzungukayo kama vile dini, siasa na matabaka. Wadau wakubwa wa fasihi linganishi kwa wakati huo walikuwa ni watu binafsi waliofanya kazi kipwekepweke. Watu hao kwa uchache ni pamoja na Paul Van Tieghen ambae aliandaa makongamano huko Sarbonne kati ya mwaka 1827-1840, yeye aliandika makala na vipeperushi kuhusu dhana ya fasihi linganishi na kuvisambaza sehemu mbalimbali huko Ulaya. Wengine ni Dostoevsky na Marius Franco.

Kuhusu maana ya Fasihi Linganishi, wataalamu mbalimbali wametoa fasili kuhusu dhana hii. Miongoni mwa wataalamu hao ni Totosy de Zepetnek (1996), ambaye anasema kuwa, Fasihi Linganishi ni taaluma inayojihusisha na uteuzi na uchambuzi wa vipengele mbalimbali vya kazi za fasihi, kama vile kanuni, mafundisho na tamaduni ambavyo vinapatikana katika kazi za fasihi za jamii mbalimbali. Totosy de Zepetnek (1998) anaeleza kuwa Fasihi Linganishi ni taaluma ya ulinganishi wa tamaduni na asili za jamii mbalimbali, pia ulinganishi wa taaluma za sayansi na taaluma nyinginezo zinazohusu tamaduni, filamu, fasihi, habari na mawasiliano. Bassnett (1993) kwa upande wake anaeleza kuwa fasihi linganishi ni taaluma ya usomaji matini za taaluma tofauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana.

Wamitila (2003) na Jilala (2016) wanaitazama dhana ya fasihi linganishi ambapo wanasema kwamba ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kueleza sifa za mfanano zilizopo katika matini ya fasihi na kwamba, dhana yenyewe huenda sambamba na

dhana ya ulinganuzi, ambapo ulinganuzi ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kuonyesha sifa zinazotofautisha baina ya matini zaidi ya moja za kifasihi. Taaluma ya Fasihi linganishi huangalia mambo anuai yanayotakiwa kufanyiwa ulinganisho wa vipengele vya kisanaa. Shughuli zote hizo hufanywa katika nyanja kuu tatu. Ponera (2014) anazitaja nyanja hizo kuwa ni nyanja ya uhakiki linganishi, nyanja ya uhusishaji wa kazi za fasihi na uasili na uhalisi na nyanja ya uhusishaji wa fasihi na sanaa nyinginezo. Kwa kutumia maeneo au nyanja hizo vigezo vya ulinganisho hufanyiwa ulinganisho. Vigezo hivyo vya ulinganisho ni pamoja na kigezo cha maana, uwakati, uigaji na uathiriano, upokezi, unusura, ukanda, fani, maudhui, motifu na utamaduni.

Kutokana na fasili hizo za wataalamu kuhusu dhana ya fasihi linganishi, tunaona kuwa mawazo yao hayatofautiani katika mtazamo na mwelekeo juu ya dhana hii. Kwa ujumla, tunakubaliana na mawazo yao kuwa, Fasihi linganishi ni taaluma inayojishughulisha na ulinganishaji wa kazi za fasihi, ili kubainisha kutofautiana na kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii na kimataifa.

Pia, tumeona kuwa kutokana na mbinu zake, Fasihi linganishi huweza pia ikatumika kulinganisha kazi za fasihi za lugha tofauti, mfano fasihi ya Kiingereza, Kijapani, Kijerumani, Kichina, Kiswahili na nyinginezo, lakini huweza pia ikajishughulisha na fasihi ya lugha moja ikiwa kazi hizo asili yake ni nchi tofauti au utamaduni tofauti ndani ya lugha hiyo kama mawazo haya yanavyoshadadiwa na Jilala (2016), huku akionesha namna ulinganishaji huo unavyoweza kufanyika.

Halikadhalika kazi za fasihi za mwandishi mmoja zilizoandikwa katika kipindi kimoja ama katika vipindi tofauti vya kihistoria zinaweza kulinganishwa kwa kutumia fasihi linganishi. Kwa kuegemea katika dhana hiyo, utafiti huu utalenga kulinganisha kazi za fasihi za msanii mmoja, ili kuona kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya korasi katika kazi za msanii teule. Maarifa haya yametumika ili kulinganisha tamthiliya mbili Emmanuel Mbogo, zilizotungwa ambazo ni; *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane* na *Samora*. Lengo kuu likiwa ni kubaini jinsi msanii huyo anavyofumbata mbinu ya matumizi ya korasi na jinsi korasi ilivyotumika katika kuibua dhamira za tamthiliya hizo. Maelezo kuhusu dhana ya fasihi linganishi yametusaidia kuelewa fasili ya dhana ya fasihi linganishi, nyanja na vigezo vya ulinganisho.  Kwa mantiki hiyo imetuwezesha kuelewa kigezo cha ulinganisho katika utafiti wetu, ambapo kilitumiwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya korasi katika tamthiliya teule.

## 2.3 Dhana ya Korasi

Dhana ya korasi imeelezwa kuwa ni dhana iliyokuwa ikitumiwa na Wayunani wa kale katika shughuli zao za matambiko ya kijadi ambayo walikuwa wakiyafanya. Katika kuielezea dhana hii ya korasi Smpson na Weiner (1979), kama wanavyonukuliwa na Mutembei (2012:8) wanaielezea korasi kuwa ni kikundi cha waimbaji na wachezaji katika sherehe za kidini na sanaa za maonesho za Uyunani ya kale. Maana hii inadokeza msingi wa kihistoria kuhusu dhana ya korasi jinsi ilivyokuwa ikitazamwa katika jamii ya wayunani. Hata hivyo ni dhahiri kwamba maana hii ya korasi inaufinyu fulani kwani dhana ya korasi leo hii katika mkabala wa

kifasihi ni zaidi ya kikundi cha waimbaji na wachezaji katika sherehe za kidini na sanaa za maonesho.

Mtazamo huo ndio uliowafanya wataalamu na watafiti mbali mbali kuanza kuitazama dhana hii ya korasi kwa jicho la ndani zaidi. Kwa mfano, Webster (1961:471) wanaeleza kuwa korasi ni kikundi cha waimbaji au waongeaji ambapo wanaeleza kuwa ile dhima ya awali iliokuweko katika Uyunani ya kale sasa ilianza kubadilika kwa hali hiyo wanaeleza kuwa dhima ya korasi sasa ilikuwa ni ile ya wahusika katika kitendo na wafasiri wa kitendo. Aidha, Webster (1986) wanasema kuwa dhana ya korasi inawiyana na neno la “Kilithunia” lenye maana ya “kisababishi” wanaeleza kuwa neno “zaras” lenye maana inayokaribiana na neno korasi ni dhana inayofafanua hali ya kusababisha jambo au kulifanya litokee (Mutembei, 2012:8-9).

Saidensticke (2005) anaeleza kuwa shughuli ya tambiko iliyojuilikana kama “dithirambu” watambaji walijitokeza huku wakiimba kwa sauti moja huku wakiongozwa na uimbaji wa kikorasi. Shuguli hii ya utambikaji ilihusu jamii nzima ikawa ndio desturi ya ufanyaji matambiko yaliyomhusu kila mtu. Hivyo, kila mtu akawa ni sehemu ya korasi na akihusika katika kuimba na akishiriki kuwa sehemu ya jamii kwenye tambiko kwa mungu wao “Dionizi.”

Maelezo hayo hapo juu ya Saidensticke (kashatajwa) yametusaidia kupata uelewa juu ya jinsi ilivyochukuliwa dhana hii ya korasi katika jamii za kale na hivyo ni dhahiri kuwa matukio yaliyotajwa ambayo ni matukio ya kijamii ndio yaliyochorwa

kama ni korasi tu jambo ambalo kwa sasa wazo hili pia linachukuliwa kama ni sehemu moja tu ya korasi.

Mutembei (2012) anawanukuu Ensaiklopedia wakieleza kuwa uhusiano wa dhana ya kucheza na kuimba katika korasi unatokana na neno la Kiyunani `xopos` linalomaanisha mahali pa kuchezea. Kimsingi Mutembei anaeleza kuwa dhana ya korasi inapasa kuangaliwa katika mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni kuiangalia korasi "kidayakronia" na mkabala wa pili ni kuiangalia korasi "kietimolojia." Mutembei (kashatajwa), anaieleza dhana hii kuwa iliibuka katika uimbaji wa kimatambiko kwa upande mmoja na ilijidhihirisha katika usanii wa Kiyunani ambao huenda sambamba na mchango wa "Aeschylos" ambaye aliigiza katika sanaa za maonesho na hasa katika drama za kitanzia.

Kihistoria korasi ilikuwepo hata kabla ya michezo ya kuigiza ambayo ilitokana nayo na kwa hakika korasi ilitakiwa iwe kama ilivyokuwa mwanzoni; yaani kundi lililoteuliwa kuisema jamii nzima (Brown, 1969:56). Mawazo haya ya Brown hapo juu tunaona kuwa pamoja na kutudokeza hali halisi ya korasi katika historia, mawazo hayo yalitusaidia sana katika uchambuzi wetu lakini pia kwa upande mwengine hatuwezi kuyachukulia kuwa korasi ni kikundi cha watu tu ambacho kinadhima ya kuisema jamii kwani kwa sasa dhana hii ya korasi imetanuka kuliko ilivyochukuliwa katika mikabala ya kimapokeo.

Kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, korasi ni nadharia mpya ya uhakiki wa fasihi katika fasihi ya Kiswahili ambapo kwa muda mkubwa wahakiki wengi waliichukulia maana ya korasi kwa ufinyu mkubwa. Kwa mfano, Masoko na Mdee (1984:53),

walieleza kuwa korasi ni kiitikio. Maana hii ilikuwa ni finyu sana kwani kiitikio ni kipengele kimoja tu cha korasi ambacho kipengele hicho hujitokeza zaidi katika ushairi. Tukichukulia korasi kwa mkabala huu tunaifinya na kuifanya isijitokeze katika tanzu nyengine za fasihi kama vile riwaya na tamthilia ispokuwa pale ambapo kuna matumizi ya ushairi uliobeba kituo. Senkoro (1988:90), kama alivyonukuliwa na Mutembei (2012:6), ameiita korasi kuwa ni mkarara. Maana hii pia imejikita katika utanzu wa ushairi ambao utanzu huu hujumuisha tenzi, mashairi na nyimbo ambapo mkarara umechukuliwa kwa dhana ya kukariri au kurudia rudia. Maana hii iliyotolewa na Senkoro, inayohusu dhana ya korasi, tunakubaliana na mawazo ya Mutembei (kashatajwa) kuwa dhana hiyo ina maana finyu kwani imejikita zaidi katika fani na kuitenga kabisa maudhui.

Hivyo, baada ya kudurusu mawazo mbalimbali ya wataalamu juu ya dhana ya korasi, tunaweza kusema kuwa korasi ni matendo, fikra au maneno ya kisanaa ayatendayo mtu mmoja au zaidi katika kazi ya kifasihi au kuhusiana na kazi hiyo ya kifasihi ambapo hadhira hushirikishwa au huifanya hadhira au msomaji wa kazi hiyo atafakuri juu ya undani wa kitendo au maelezo hayo. Maneno hayo yaweza yakawa ya kinudhumu au kinathari. Aidha, matendo hayo yaweza kuambatana na maneno au bila ya matumizi ya maneno.

### 2.3.1 Aina za Korasi

Baada ya kueleza dhana ya korasi kama inavyohusishwa katika fasihi, ni vyema kuelezea aina mbalimbali za korasi kama aina hizo zilivyojadiliwa na Mutembei (2012). Kama tulivyosema hapo kabla kwamba katika kazi hii mjadala wetu uliegemea uainishaji wa korasi kama ule unaofanywa na Mutembei kwa sababu

tunaona kuwa ametoa utoshelevu wa aina za korasi katika mtazamo mpya. Aina hizo za korasi zimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 2.3.1.1 Korasi kama Mhusika

Kwa mujibu wa Kinunda (2010:54) wahusika ni watu wanaobeba majukumu mbali mbali katika hadithi (Riwaya na Tamthilia) ambao wahusika hawa wanaweza kuwa watu au wanyama ambao hubeba tabia za binaadamu.Tunakubaliana na maelezo ya Kinunda (kashatajwa) kwa upande mmoja na tunasema kuwa wahusika ndio kipengele ambacho katika nathari ni nguzo kuu katika kubeba dhamira za mwandishi wa kazi husika. Aidha, muandishi huwa anawatumia wahusika ili kupeleka mbele matukio ya kazi husika. Korasi kama mhusika ilizuka baada ya kuibuka kwa sanaa na matendo ya dhati yaliyoongozwa na korasi. Waigizaji walianza wakiwa wengi na kadri muda ulivyopita wahusika walipunguwa. Hivyo korasi kama kikundi cha wahusika, kikundi hicho kilipunguwa hata kufikia mtu mmoja tu ikachukuliwa kuwa ni korasi. Kwa hali hiyo, dhana ya korasi kama mhusika inaweza kuwa kundi la wahusika au mtu mmoja tu ambaye amekuwa akisimulia hadithi, akiuliza maswali au akitoa maelekezo au akiunganisha kati ya tukio moja na jengine wakati wahusika wanapobadilisha mavazi nyuma ya pazia (Brocket, 1991).

Mutembei (2012:43) akifafanuwa dhana hii ya korasi kama mhusika anaeleza kuwa mhusika wa korasi alikuwa ni mhusika katika mchezo akitoa ushauri, akitoa maoni, akiuliza maswali na wakati mwengine akiwa mtendaji wa mara kwa mara katika mchezo, akishiriki kikamilifu katika mchezo, na akiongoza muelekeo wa onesho zima. Mawazo haya ya (Brocket, 1991) na Mutembei (2012), yalikuwa na manufaa makubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu uchambuzi huo wa korasi kama

mhusika umeingia ndani na kutoa taswira halisi ya namna ya kufanya uchambuzi wa korasi kama mhusika katika kazi za fasihi. Tumebaini kwamba mhusika anaweza kutazamwa kama korasi pale ambapo anauliza maswali, anatoa maelekezo, anaunganisha tukio moja na jengine katika hadithi ama kile kinacoelezwa. Kwa mantiki hii mawazo haya yalichukuliwa na mtafiti ambapo yalisaidia kudondoa data zinazohusiana na korasi kama mhusika katika tamthilia teule.

#### 2.3.1.2 Korasi kama Tukio la Mila na Desturi

Korasi kama tukio la kijamii, inaelezwa na Mutembei (2012:5), kuwa ni tukio la kijamii ambalo lilihusisha jamii nzima. Sanaa na utendaji wa kikorasi ulionekana katika kila sekta ya maisha ya Wayunani kwa ujumla wao. Yawe maisha ya kidini, yasiwe ya kidini, ya mtu binafsi au ya umma. Utokeaji huu ulifanya maisha ya kiyunani uwe wa kikorasi. Maelezo haya ya Mutembei (kashatajwa), yametupatia mawazo muhimu ya namna ya kuichunguza dhana ya korasi kama tukio la kijami. Kwa hivyo, mawazo haya yalichukuliwa na mtafiti ili kuona iwapo yamejitokeza katika tamthilia au hayakujitokeza.

#### 2.3.1.3 Korasi kama Mtindo

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (2008:47) mtindo ni ufundi wa kupanga na kupanguwa, na pia ni ujuzi wa kujieleza. Mtindo hutumiwa kupeleka mbele dhamira pamoja na kusanifu kazi nzima ili ufasaha ujitokeze.Maelezo haya ni muhimu sana katika kazi yetu. Mawazo haya yalisaidia kutupatia mawazo ya kufanya uchunguzi wa kipengele cha korasi kwa kutumia kigezo cha mtindo. Hivyo kutokana na maana ya mtindo kama ilivyotolewa na Njogu na Chimerah (kashatajwa) tunaweza kusema kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na mtindo fulani ambao mtindo huo utasaidia

kupeleka mbele kazi hiyo na hivyo muandishi kuweza kukifikisha kile anachotaka kuifikishia jamii yake. Kile ambacho tunaona tukisisitize ni kwamba muandishi mmoja na mwengine hutofautiana katika kufikisha ujumbe, utofauti huu ni ule mtindo atakaoutumia.

Korasi kama mtindo imeelezwa na Brocket (1991), katika Mutembei (2012), kwamba hujitokeza kwa kuumba mazingira ya mchezo kwa ujumla nayale ya kila onesho na ukuzaji wa athari ya tamthiliya. Hapo kabla korasi kama mtindo ilikuwa kama ridhimu ikitokeza mapumziko na mwendo wa matukio kutokana na mapumziko hayo maana ya kazi iliweza kujuilikana. Aidha, korasi kama mtindo hujitokeza kuwa ni kiunganishi cha matukio na hadithi ambacho pasi na kuwepo hakuna hadithi inayoweza kusimama peke yake na kukamilisha maana. Robert (2005), ananukuliwa na Mutembei (2012:38) akisema kuwa korasi kama mtindo inaangaliwa kuwa ni kiunganishi cha matukio na kwa kufanya hivyo kilileta maana ya tukio au mchezo mzima. Aidha, korasi sio tu matukio yaliyopita ambayo huweza kuoneshwa lakini pia huweza kufanya uunganishaji usiotarajiwa na ambao ni changamano wa matukio hayo. Unaweza kuwa uunganishaji unaofanywa na sauti tu, mawazo ya muandishi au wahusika.

#### 2.3.1.4 Korasi kama Dhamira

Kwa mujibu wa Mbunda (1992:44) na Madumulla (2009:136) korasi kama dhamira hupatikana kwa kupitia wahusika na dhima wanazozibeba. Wahusika hawa wanaweza kuwa wahusika wakuu na hata wahusika wadogo na huweza kujenga dhamira mbali mbali zinazojitokeza katiaka kazi nzima. Mhusika mdogo dhima yake na umuhimu wake katika ujitokezaji wa dhamira na maana nzima ya kazi ya fasihi

husika, ni mdogo au haupo kabisa. Kwa mujibu wa nadharia ya korasi mhusika mdogo anaweza kutamka ikawa ni korasi yale maneno yake na yeye mwenyewe akawa korasi (Mutembei, 2012:50).

#### 2.3.1.5 Korasi kama Wimbo

Kwa mujibu wa Mutembei (2012:31) korasi kama wimbo imekuwa ikifafanuliwa kupitia maana ya muziki. Korasi kama wimbo inaelezwa kuwa ni watu wanaoimba katika umoja. Uimbaji huu unawahusisha waimbaji na ala za muziki katika tukio la sanaa za maonesho. Akiendelea kufafanua dhana ya korasi kama wimbo, Mutembei (kashatajwa) anaeleza kuwa korasi kama wimbo ieleweke kuwa pia huwa inaweza kujitokeza kama ni sauti inayotoka mara kwa mara ikimrudisha nyuma msikilizaji au ikimpeleka mbele ya tukio kumuonesha kama utabiri wa yale yatakayotokea. Inaweza kuwa ni sauti ambayo inaweza kuja na kumtolea msomaji au msikilizaji ujumbe ambao haukuoneshwa na wala hautaoneshwa na masimulizi yaliomo. Maelezo ya korasi kama wimbo yaliyotolewa na Mutembei (kashatajwa), yanaweka wazi namna ya kutambua matumizi ya wimbo ambao unafanya kazi kama korasi. Mawazo haya yametupatia uelewa kwamba nyimbo ziliomo katika kazi za fasihi kama vile tamthilia hutumika kama korasi pale zinapomdokezea msomaji au msikilizaji kile kitakachoelezwa huko mbele iwapo wimbo huo umejitokeza mwanzoni. Ama ikiwa wimbo huo umejitokeza mwishoni mwa kazi husika hutumika kama muhtasari wa kueleza kile kilichozungumziwa na mtunzi kabla ya wimbo huo. Hivyo basi, mtafiti aliyachukuwa mawazo haya ili kufikia lengo la utafiti huu.

#### 2.3.1.6 Korasi kama Muundo

Mutembei (2012:39-40) akimnukuu Brocket ambaye aliieleza kuwa korasi kama muundo ni kikundi cha waimbaji na wachezaji wachezao kwa pamoja na kuwa washiriki au kutoa maoni katika onesho (1991:27). Anaendelea kueleza kuwa dhana mbili muhimu katika kujenga uelewa juu ya korasi ni uimbaji au uchezaji kwa pamoja na kushiriki katika onesho au kutoa maoni kuhusu onesho. Muundo huo ulifanya dhana ya wahusika na waigizaji kubadilika badilika. Jambo hili linahusu muundo na pia linagusia mtindo. Ikumbukwe kuwa korasi kama muundo iliingizwa katika tamthilia kama mtindo, kama muundo na baadae kabisa kama mhusika (Mutembei, 2012:42). Mawazo haya yanayohusu korasi kama muundo yanaonesha kuwa dhana hii ni changamano kwani huweza kukusanya vipengele tofauti kama vile mtindo, kama muundo na kama mhusika. Hata hivyo, tumepata uelewa kuwa vipengele hivi vya kifani huweza kutumika kuwa ni korasi kama muundo pale inapojenga muundo wa mshikamano wa visa na matukio ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara. Kwa mantiki hii tunasema kuwa mchambuzi wa kazi ya fasihi kwa mkabala wa kikorasi inampasa awe makini zaidi ili kuibua kwa usahihi vipengele vilivyotumika kuwa korasi kama muundo. Hivyo, maelezo haya pia yatatuwezesha kutambua namna ya kukusanya data zinazohusiana na korasi kama muundo katika tamthilia teule.

#### 2.3.1.7 Korasi kama Kimya

Kwa mujibu wa Mutembei (2012:57-61) anaeleza kuwa tunapozungumzia korasi kama kimya ni vyema kurejelea maana pana ya korasi. Maana hiyo pana inaeleza dhana hii ya korasi kuwa ni matendo, fikra, maneno ya kisanaa ayatoayo mtu au

watu ndani ya sanaa au ayatoayo kuhusiana na kazi ya kisanaa ambayo hadhira hushirikishwa au hufanya ifikiri undani wa kitendo fikra au maneno hayo jinsi ambavyo isingelifanya kama ingelikuwa vyenginevyo. Jambo hili linagusa muitikio wa msomaji, msikilizaji na mtazamaji wa kazi husika ya kisanaa. Katika upana wake matendo hayo ya kisanaa yaweza kuambatana na ukimya au ububu. Hapo basi korasi itapimwa kutegemea muitiko wa msomaji au mtazamaji. Sauti ya kimya yenye maana sana ni ile inayojenga ushawishi. Aina hii ya kimya ndiyo tuliyoitumia katika uchambuzi wetu kwani ndio inayobeba maana ya kikorasi.

Namna nyengine ya kimya ni ile ya kimya kiletwacho na ujenzi wa fikra za mwanaadamu kutokana na jambo au neno lililosemwa au kinyume au nusu yake au sehemu yake tu. Msemaji wa awali huacha kwa makusudi kusema jambo fulani ili kuziruhusu fikra za wale wanaomsikiliza zitalii na kuibua maana anuai. Msemaji wa awali anaamua kusema neno bila kulimaliza , kutaja kifungu cha maneno na kuacha kifungu chengine au hata kusema kinyume na kile kinachotarajiwa ili kutokana na ukimya wake huo kutapelekea kuziamsha fikra za wale wanaosoma au kusikiliza. Korasi kama kimya huweza kujitokeza, kwanza kimya kinachotokana na sababu za kiutamaduni ambapo mtunzi inamfanya asieleze baadhi ya mambo wazi wazi kutokana na kutoa taswira ya karaha. Mathalani, kusimulia matendo ya ngono wazi wazi. Aina ya pili ya korasi kama kimya  hutokana na kimya cha kulazimishwa ambacho husababishwa na mtunzi kuhofia rungu la utawala kueleza wazi wazi baadhi ya mambo.

Maelezo haya ya korasi kama kimya yameingia ndani zaidi na kutupatia uelewa wa namna aina hii ya korasi inavyoweza kujitokeza katika kazi za fasihi. Hivyo,

muongozo huo ulitumika ili kuona ni jinsi gani mtunzi amefanikiwa kutumia korasi kama kimya katika kazi teule na namna kimya hicho kilivyotumika kuibua dhamira za mtunzi.

Kwa kuzingatia malengo, maswali na mada ya utafiti huu, mtafiti amekusudia kutumia aina hizi za korasi: Korasi kama wimbo, korasi kama kimya, korasi kama muhusika, korasi kama mtindo, korasi kama muundo, korasi kama mila na desturi na korasi kama dhamira. Aina hizo zimetumika kuwa mbinu za kikorasi katika tamthiliya teule. Sambamba na hilo aina hizo za korasi kutumika kuwa mbinu za kikorasi ndio msingi wa uwasilishaji na uchambuzi wa mada ya utafiti kwa kurejelea tamthiliya teule za: *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora.*

## 2.4 Utafiti linganishi katika Tamthiliya ya Kiswahili

Jilala (2016) anasema kwamba fasihi linganishi ni taaluma kwa sababu inahusu misingi ya kinadharia mbinu na kanuni mahususi. Katika taaluma ya fasihi linganishi vipengele vya fani na maudhui hutumika kulinganishwa. Kama nadharia inajihusisha na nadharia, mbinu na vitendo. Fasihi linganishi hujihusisha na vipengele vitatu katika mchakato wa ulinganishaji. Vipengele hivyo ni fani, maudhui na utamaduni isimu. Watafiti mbalimbali wamefanya utafiti linganishi kuhusu tamthiliya ya Kiswahili. Baadhi ya tafiti hizo zimejikita katika kulinganisha na kulinganua vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya moja na nyingine au baadhi zimechambua dhima ya mtindo katika tamthiliya kwa kufanya utafiti linganishi. Baadhi ya kazi zilizojihusisha na kuchunguza vipengele vya fani na maudhui kwa mkabala wa fasihi linganishi ni kama zifuatazo:

Saleem (2013) alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kulinganisha na kulinganua vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya hizo na hatimaye kubainisha sababu za mfanano na utofauti katika vipengele hivyo. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa kufanana na kutofautiana kwa tamthiliya hizo kumetokana na tofauti katika mbinu za kimtindo walizozitumia waandishi katika kujenga kazi zao.

Utafiti wa Saleem (kashatajwa) ulikuwa na manufaa makubwa katika kufikia lengo la utafiti huu. Hii ni kwa sababu mtafiti alijifunza namna data zinazohusiana na utafiti linganishi zinavyofanyiwa uchambuzi na namna zinavyowasilishwa. Hata hivyo utafiti huo ulikuwa na tofauti na utafiti wetu kutokana na Saleem kulinganisha tamthilia za waandishi wawili tofauti lakini sisi tulilinganisha kazi za mtunzi mmoja. Aidha, utafiti huu haukujikita katika kuchunguza fani na maudhui bali umechunguza matumizi ya korasi katika kazi za fasihi za mtunzi mmoja jambo ambalo Saleem hakulishuhulikia kwa sababu halikuwa lengo la utafiti wake.

Mkuwili (2014) alifanya utafiti linganishi kuhusu fani na maudhui katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Kivuli Kinaishi.* Lengo la utafiti wake ilikuwa ni kuchunguza jinsi waandishi wanaotoka katika maeneo tofauti ya kijiografia yaani pwani na bara wanavyofanana na kutofautiana kifani na kimaudhui. Kwa kuwa utafiti huo ni utafiti linganishi, ulitusaidia kubaini mbinu na nadharia ya fasihi linganishi katika kulinganisha kazi za fasihi. Tofauti ya utafiti huo na utafiti huu ni kutokana na malengo ya utafiti pamoja na kutumia Nadharia ya Korasi ambayo yeye hakuitumia. Lengo la utafiti huu ni kubaini jinsi msanii teule anavyofumbata matumizi ya mbinu ya korasi.

Fadhili (2014) amefanya utafiti linganishi kuhusu dhima ya mtindo katika tamthiliya za kihistoria za *Morani* (1993) na *Kinjeketile* (1969). Katika utafiti wake amechunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya hizo ili kuona ni jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo wanafanana na kutofautiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo wanapowasilisha suala la kihistoria. Utafiti huo umegusia vipengele vya lugha ambavyo pia ni matini zilizoshughulikiwa na utafiti huu, hivyo utafiti huo ulikuwa ni wenye manufaa kwetu kwa kubaini namna vipengele vya kifani vianavyohusiana na korasi vinavyoweza kufanyiwa uchambuzi. Hata hivyo utafiti wetu ni tofauti na utafiti huo kwa sababu utafiti wa Fadhili (kashatajwa) haukujikita katika kuchunguza matumizi ya korasi. Pia, haukutumia nadharia ya korasi. Kwa maana hiyo tafiti hizi ni tafiti mbili tofauti zenye malengo tofauti.

Jilala (2016) alifanya uchambuzi wa kazi mbalimbali za fasihi kwa mkabala wa fasihi linganishi. Katika kazi hizo alifanya ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi za lugha tofauti na zile za lugha moja ya Kiswahili. Pia, alifanya ulinganishaji wa kazi za mtunzi mmoja.Kwa mfano alifanya ulinganishaji wa kazi za fasihi ya Kiswahili kwa kutumia mifano ya riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na riwaya ya *Tata za Asumini* (1980). Pia, Jilala alifanya ulinganishaji wa riwaya za E. Kezilahabi *Rosa Mistika, Nagona* na *Mzingile*. Kwa ujumla kazi hizi zilikuwa na manufaa sana katika utafiti wetu. Tuliweza kuona namna data zinavyochambuliwa na kuwasilishwa na hatimae kufanyiwa ulinganishaji. Hivyo tulichukuwa mawazo haya na hatimae tuliweza kukamilisha kazi yetu.

## 2.5 Tafiti Kuhusu Korasi Katika Kazi Mbalimbali

Waandishi kadhaa wamewahi kuandika kuhusu dhana ya korasi katika fasihi hasa kuhusu tamthiliya. Kazi hizi kwa kiwango kikubwa kinahusu tamthiliya za Wayunani wa kale. Baadhi ya watafiti hao tulitalii na kugundua kuwa wameshughulikia korasi katika viwango na mitazamo tafauti kama ifuatavyo:

Wikipedia (2010) wanaeleza kwamba tamthilia za mwanzo za Wayunani wa kale kama vile tanzia na tamthiliya vichekesho na hata tamthiliaza leo zimekuwa zikimtumia wahusika wa kikorasi. Wahusika hawa wamekuwa wakitoa maelekezo wakiwa jukwaani. Tangu kale korasi za Wayunani zilitumia wahusika kati ya 12 hadi 50 ambao huwa wanaimba kwa pamoja mara nyengine huwa wanavaa maleba. Maelezo haya yanayotolewa na Wikipedia yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kufikia malengo ya utafiti wetu. Kutokana na mawazo haya tuliweza kubaini namna wahusika wanavyotumiwa na msanii kama sehemu ya korasi pale wanapoimba kwa pamoja na wakati wahusika hao wanapotoa maelekezo kwa hadhira.

Salim (2015), alifanya utafiti akiwa na mada *"Kuchunguza Ufasihi Simulizi katika Riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze."* Katika utafiti huu anaelezwa kuwa riwaya ya Kusadikika imetumia mtindo wa korasi ambapo kuna kuuliza maswali katika kila mwisho wa sehemu kama kiunganishicha mawazo yaliyoelezwa nayale yanayokuja. Kazi hii ya Salim pia ilikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Kazi hiyo ilituonesha namna mtindo unavyoweza kujitokeza kama sehemu ya korasi katika kazi za fasihi. Kazi hii ilitubainishia kuwa katika riwaya kuna matumizi ya korasi.

Hishon (2016) alifanya utafiti ambapo kazi yake ilikuwa na anuani “Greek Corus.” Katika utafiti huo anaeleza kuwa lengo la korasi katika jamii ya Wagiriki ilikuwa ni kutoa utangulizi na ufupisho kwa hadhira ili kubaini kile kitakachofuata. Hili lilifanyika kwa sababu tamthiliya za Wagiriki zilikuwa refu. Utafiti huu ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba tulichunguza namna korasi katika tamthiliya teule zilivyotumika kuibua dhamira. Pia, tulipoziona nyimbo ama wahusika katika jukwaa tuliangalia kwa kina ni jinsi gani zilivyotumiwa na msanii kama muhutasari wa tamthiliya teule.

Vile vile, Oberheiden (2009) alifanya uchunguzi wa korasi katika tamthiliya ya Shakespeare. Katika utafiti huo mada yake ilikuwa “The Role of the Chorus in Shakespeare`s Henry V.” Katika utafiti huo aligundua kwamba katika tamthiliya hiyo Shakespeare ametumia korasi ikiwa na dhima kuu mbili. Dhima ya kwanza ni kuiongoza hadhira katikka kupata kile kinachozungumzwa. Dhima ya pili ni kumtambulisha Mfalme Henry V ili msomaji kutambua tabia ya mhusika huyu. Utafiti huu ulikuwa na manufaa katika kufikia lengo la utafiti wetu. Hii ni kutokana na kwamba tuliweza kuona namna data zinazohusiana na korasi zinavyoweza kujitokeza na kufanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa katika utafiti. Pia, tuliona namna korasi zinavyoweza kujitokeza zikiwa na dhima mbalimbali. Kutokana na kazi hiyo tumebaini namna korasi zinavyoweza kuibua dhamira katika kazi za fasihi.

Pia, Bachelora (https://www.bacheloranamaster.com), alifanya utafiti akichunguza dhima za korasi katika tamthiliya ya *Oedepus Rex*. Utafiti huu ulikuwa na anuani inayosema “The Role of Chorus in Oedipus Rex.”Katika utafiti huu Bachelora aligundua kuwa dhima ya korasi katika tamthiliya *Oidepus Rex* ni kuimba kwa

pamoja ambacho wimbo uliomo unaonesha kile kitachotokea baadae. Pia, korasi katika tamthiliya hiyo imetumiaka kuonesha uhalisia wa maisha ya jamii, kutathmini matukio, maendeleo ya wahusika na dhamira za tamthiliya hiyo. Vile vile, korasi imetumika ikiwa na dhima ya kuongeza hisia, majibu na uelewa wa hadhira. Korasi ziliomo katika tamthiliya hii zinatueleza kipi cha kusema, cha kufanya na kutathmini kile kile kinachotendeka jukwaani. Utafiti huo pia ulikuwa na umuhimu mkubwa katika kusukuma mbele utafiti huu. Hii ni kwasababu tulipata uelewa wa kina juu ya korasi katika kazi za fasihi. Hivyo mawazo haya tuliyachukua na hatimae kujibu maswali ya utafiti huu.

Mutembei (2012) alifanya uchambuzi wa korasi. Katika kazi yake anafanya uvumbuzi wa namna korasi inavyoweza kutazamwa katika mtazamo mpya wa kihakiki. Mutembei anayataja matapo ya korasi ambapo anasema kuwa kuna korasi kama mhusika, korasi kama tukio la mila na desturi, korasi kama dhamira, korasi kamakimya, korasi kama wimbo, korasi kama mtindo na korasi kama muundo. Mutembei aliweza kuzifafanua aina hizi za korasi huku akidondoa mifano katika kazi za fasihi ili kushadadia yale anayoyaeleza. Kwa kufanya hivi aliweza kuonesha uchambuzi wake kwa misingi ya kisayansi. Kazi hii ya Mutembei (khj) ilikuwa ni muhimu sana katika kazi yetu. Tuliitalii miktadha ya korasi kama alivyoifanyia uchambuzi. Kutokana na utalii wa kazi hii tulipata uelewa wa kina ambao ulituwezesha kuzigawa data zetu katika matapo ya korasi kama yale yanayobainishwa na Mutembei. Pia, tuliona namna ya kufanya uchambuzi na kuwasilisha vipengele vya korasi kwa miktadha ya kifasihi.

## 2.6 Pengo la Utafiti

Kazi kadhaa tumezitalii zinazohusu korasi katika kazi za fasihi. Tumebaini kwamba watafiti wengi wamewahi kufanya utafiti kuhusu tamthiliya za Emmanuel Mbogo wakijikita katika vipengele vya fani na maudhui. Pamoja na kazi hizo katika utalii uliofanyika mtafiti hakuona kazi iliyotafiti moja kwa moja matumizi ya korasi katika tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* kwa mkabala wa fasihi linganishi. Hivyo basi, utafiti huu ulifanyika kwa lengo la kuchunguza matumizi ya mbinu za korasi katika tamthiliya teule kwa mkabala wa fasihi linganishi ili kubaini namna E. Mbogo amekuwa akitumia mtindo wa korasi katika kusana tamthiliya zake.

## 2.7 Mkabala wa Nadharia

Njogu na Wafula (2007) wanasema nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum. Msokile (1993) anafafanua maana ya nadharia kwa kusema kwamba ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Kila nadharia huwa ni muhimu na yenye ubora na mapungufu yake. Uteuzi wa nadharia bora inategemea uteuzi wa mtafiti kwa mujibu wa mada, malengo na maswali ya utafiti wake. Hivyo basi, utafiti huu umekusudia kutumia nadharia ya Korasi na nadharia ya Fasihi Linganishi. Msingi mkubwa wa kuchagua nadharia hizi ni imani ya mtafiti ya kwamba nadharia hizi zitaweza kufanikisha malengo na mwisho kujibu maswali ya utafiti huu. Nadharia hizo zimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

### 2.7.1 Nadharia ya Fasihi Linganishi

Nadharia ya Fasihi Linganishi inahusishwa sana na Zepetnek. Zepetnek (1998) anaifafanua Nadharia ya Fasihi Linganishi kama nyenzo ya kuyachanganua na kuyashughulikia masuala ya ulimwengu. Kwa mtazamo huu, taaluma hii huweza kuelezwa kwa namna kuu mbili. Kwanza ni utambuzi wa maarifa yahusuyo lugha na utamaduni wa taifa zaidi ya moja na kuchunguza jinsi ambavyo maarifa hayo yanavyotumiwa katika kuustawisha uga wa fasihi. Pili, ni taaluma ambayo stadi zake zimeelekezwa katika itikadi ya kuzijumuisha fasihi zote za ulimwenguni, pamoja na tanzu ambazo hazipewi umbele au hazichangamkiwi sana katika kushughulikiwa. Ponera (2014) na Mlaga (2017) wanaeleza kuwa chimbuko la dhana ya fasihi Linganishi liko katika maneno ya Kifaransa, yaani `*la Literature Comparee*` yenye maana ya `*Fasihi Linganishi*` kwa Kiswahili. Baadae huko huko Ulaya dhana hii ilipewa majina mbali mbali kulingana na vipindi vilivyopitia. Miongoni mwa majina hayo ni “Fasihi Linganishi ya Kihistoria”, “Fasihi Linganishi ya Kisasa” na “Fasihi Linganishi ya Kimataifa”.

Fikra za kulinganisha fasihi za jamii au mataifa mbali mbali ni za kale ikilinganishwa na sura ya ulinganishaji ilivyo hivi sasa kama nyanja ya kitaaluma. Kabla hata ya kuifanya dhana hii ya fasihi linganishi kuingizwa katika hali na hadhi hii ya kitaaluma tayari kulikuwapo na misingi kadhaa ya kikanuni iliyokuwa inafuatwa na jamii hizo katika kulinganisha utendekaji wa fasihi zao na za jamii nyengine. Misingi hiyo ilikuwa inaongozwa na vionjo vya jamii zilizokuwa na nguvu ya kihadhi kama vile; jamii za Wayunani. Mathalani, zama za mwanafalsafa wa Kiyunani, Aristotle

zilishuhudia kuwapo kwa ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi mbali mbali za tamthilia kwa lengo la kuchuja na kupata kazi bora zilizowafikiwa kupelekwa kwa hadhira. Pia, jamii za zama baada ya Kristo zilijihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa matini za kidini (Biblia). Kadhalika, wasanii wa Kiarabu wa enzi za kati walijishughulisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi za kisanaa. Hata hivyo, pamoja na kufanya mambo mengi yanayohusiana na ulinganishaji wa kazi za kisanaa katika zama hizo ni wazi kuwa suali lenyewe lilifanywa kwa misingi isiyo rasmi.

Fasihi linganishi katika umbo la sasa la kitaaluma, ilianza mwishoni mwa karne ya 19 na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya 20. Kiusuli, kuibuka kwa dhana ya kufanya ulinganisho katika vipengele mbali mbali vya kifani kunanasibishwa na safari zilizokuwa zinafanywa na wataalamu mbali mabali katika sehemu tofauti za dunia. Ijapokuwa madhumuni ya safari hizo ilikuwa si kwa madhumuni ya kuzitalii fasihi au sanaa za sehemu hizo, bali ilidhihirika kuwa kulikuwa na tofauti fulani walizozibaini katika utendekaji wa fasihi na sanaa kwa ujumla, hususani fasihi simulizi.

Maarifa ya awali ya taaluma hiyo yalijikita katika kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na mambo yamzungukayo kama vile dini, siasa na matabaka. Wadau wakubwa wa fasihi linganishi wa mwanzoni walikuwa ni watu binafsi wachache kama vile Paul Van Tieghem wa Ireland aliyeendesha makongamano huko Sorbonne kati ya mwaka 1827 na 1840. Wengine ni Dostoevsky na Marius Franco ambao walijitokeza katikati ya miaka ya 1800. Nadharia hii kwa miongo kadhaa inatumika kufanyia uchambuzi wa kazi za kifasihi hasa katika bara la Ulaya na Amerika. Hata hivyo, pamoja na umaarufu huo,

nadharia hii imekuwa ikikosolewa kwamba, fasihi linganishi haijitoshelezi kwa sababu ya kuchanganya taaluma mbali mbali kama vile Tafsiri, Nadharia ya Uhakiki, Anthropolojia, masomo ya Dini, Historia na Jiografia. Kwa mantiki hii inadaiwa kuwa ni rahisi sana kwa walinganishaji kuangukia katika dimbwi la unusu nusu wa maarifa.

Pamoja na kasoro hizo, nadharia ya fasihi linganishi inaonekana kuwa na ubora kutokana na kuwa ni somo la utafiti wa fasihi bila mipaka. Muono huu hutokana na matakwa ya msingi wa fasihi linganishi ambao ni kuwa na ujuzi na uwezo wa kusoma, kuandika, kuchunguza na kuhakiki hadhi ya kazi za jamii mbali mbali za kuanzia Mashariki hadi Magharibi; na Kaskazini hadi Kusini mwa dunia. Vilevile, fasihi linganishi inamtaka mdau wake azitalii kazi za vipindi mbali mbali kama vile; kazi za zama za giza hadi zile za ufufuo wa ustaarabu, za kabla ya ukoloni hadi zile za baada ya ukoloni na za urasimi mkongwe hadi zile za ulimbwende na uhalisia. Kwa sifa hizi utafiti huu umeona hauna budi ila kuitumia nadharia hii ili kufikia lengo la utafiti huu. Kimsingi nadharia ya fasihi linganishi ilitumika kufanya uchambuzi wa lengo la tatu ambalo linahusu kulinganisha na kulinganua vipengele vya korasi na dhamira katika tamthiliya teule.

### 2.7.2 Nadharia ya Korasi

Nadharia ya korasi inaelezwa na Mutembei (2012), kwamba ni nadharia ambayo ilianza huko Uyunani ya kale. Nadharia hii hapo kabla ilichukuliwa kama ni kundi la watu lililokuwa likiimba kwa pamoja. Baadae ilijumuisha kundi la watu waliokuwa wakishiriki katika matambiko yao. Hapo watazamaji na waimbaji wote kwa pamoja walichukuliwa kama sehemu ya korasi. Kwa vile mtazamo huu ulikuwa ni finyu

Diegner katika Mutembei (2012), amefanikiwa kueleza dhana ya korasi ilivyo pana katika miktadha mbalimbali ya kijamii, kitamaduni na kifasihi vile vile. Anasema kuwa dhana ya korasi ingawa inaangaziwa kutoka asili ya Wayunani panahitajika kufanyika utafiti ili kujuwa iwapo ilikuwepo Afrika miaka mingi kabla ya kuzuka katika jamii ya Wayunani; vyovyote vile iwavyo nadharia hii inaweza kutumika kufanyia uchambuzi wa tamaduni, na hasa fasihi za ulimwengu mzima ikiwemo fasihi ya Kiswahili.

Kutokana na dhana ya korasi kuangaliwa maana finyu ya kutumika kuchambua kazi za ushairi tu Mutembei ameunda nadharia inayofaa katika uhakiki ambayo huweza kutumika katika tamthilia, riwaya na ushairi.Wazo kuu la nadharia hii ni kuiangalia fani na maudhui kwa pamoja wakati wa kufanya uchambuzi wa kazi za fasihi.

#### 2.7.2.1 Misingi ya Nadharia ya Korasi

Misingi ya nadharia ya Korasi amabyo imeongoza utafiti huu ni ile inayobainishwa na Mutembei (2012) kama inavyojadiliwa katika kitabu kinachoonesha nadharia hiyo katika mkabala mpya. Hivyo misingi hiyo ilibainishwa na mtafiti kama ifuatavyo:

i. Kuwepo kwa jamii katika utamaduni wao katika maisha.
ii. Utumiaji wa maneno au matendo katika kuliwasilisha tukio la kijamii.
iii. Kuwepo kwa kikundi cha wachezaji na waimbaji katika sanaa lengwa.
iv. Muhimili mwengine ni kuwepo kwa utanzu unaotambwa (yawezakuwa mazungumzo, dialojia, ushairi na nyimboau ngoma).

### 2.7.2.2 Aina za Korasi katika Mtazamo wa Kisasa

Mutembei (2012) katika uchambuzi wake wa korasi katika fasihi amedokeza aina saba za korasi ambazo kwazo ndizo zilizotuongoza katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Aina hizo za korasi ni korasi kama wimbo, korasi kama tukio la mila na desturi, korasi kama muundo, korasi kama mtindo, korasi kama mhusika, korasi kama dhamira na korasi kama kimya. Hivyo, katika utafiti huu nadharia ya Korasi ilitumika ili kumuongoza mtafiti katika lengo la kwanza na lapili ambayo yanahusu kutathmini mbinu za korasi zilizotumika katika tamthilia teule na namna vipengele vya korasi vilivyotumika kuibua dhamira za mtunzi. Pia, nadharia ya Fasihi Linganishi ilimuongoza mtafiti katika kulinganisha matumizi ya mbinu za korasi katika kazi zilizotafitiwa. Tumechagua nadharia hizo tukiamini kwamba zitatufikisha katika malengo ya utafiti huu.

## 2.8 Hitimisho

Katika sura hii utafiti huu uliwasilisha mapitio ya kazi tangulizi ambayo yanahusiana na viatabu, wavuti na tasnifu mbalimbali ambazo zinahusiana na nada ya utafiti huu. Kwa kufanya hivyo utafiti umefanikiwa kubainisha pengo la utafiti huu. Pia, katika sura hii tumefanya uchambuzi na uwasilishaji wa nadharia ya Fasihi Linganishi na nadharia ya Korasi.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mbinu mbalimbali zilizotumika katika kufanikisha utafiti huu. Sehemu hii inaeleza vipengele kadhaa. Vipengele hivyo ni umbo la utafiti, eneo la utafiti, na mbinu zilizotumika kukusanyia data. Vipengele vingine ni mbinu za uteuzi wa data, wateuliwa, mipaka ya utafiti na vifaa vilivyotumika katika kukusanyia data.

## 3.2 Umbo la Utafiti

Utafiti huu ulitumia umbo la kimaelezo na kitakwimu. Enon (1999) anasema kuwa umbo la kimaelezo ni njia ya kukusanyia data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya kimaelezo ambapo nambari huwa hazitumiki. Hii ni kusema kuwa utafiti unaotumia umbo la kimaelezo data hukusanywa na kufanyiwa uchambuzi kwa njia ya maelezo bila kutumia tarakimu. Kwa kawaida tafiti zinazohusu maandishi ya kifasihi data zake hufanyiwa uchambuzi kwa mkabala wa kimaelezo. Salim (2015) anasema kwamba tafiti za kifasihi huegemea katika umbo la kimaelezo kwa sababu hulenga kuchunguza sanaa ya maneno. Hata hivyo ieleweke kuwa hata mkabala wa kitarakimu huweza kutumika. Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya kimaelezo na kitakwimu. Njia ya kitakwimu imetumika katika kuwasilisha data zinazohusu mdafao wa utokezaji wa korasi katika tamthiliya teule. Kwa upende mwengine njia ya maelezo imetumika kuwasilisha data nyengine zilizotumika katika utafiti huu.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la Utafiti ni mahala ambapo utafiti unafanyika kulingana na vile mtafiti anavyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali ya utafiti wake (Creswell, 2009). Eneo la utafiti huteuliwa kulingana na lengo kuu la mtafiti na kwamba hilo ni eneo au maeneo ambayo ni lazima yaweze kutoa data za kukamilisha malengo mahsusi ya utafiti wake. Kwa mujibu wa Enon (1999), eneo la utafiti la kijografia ni pahala ambapo mtafiti amekwenda au amelitumia katika kukusanya data za utafiti wake. Hivyo, utafiti huu ulifanyika katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tawi la Pemba, Maktaba Kuu Zanzibar, tawi la Pemba, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumet, Zanzibar. Maeneo hayo yalitumiwa katika kukusanya data kwasababu utafiti huu ni wa maktabani na pia mtafiti zilimwezesha kupata data za utafiti huu kwa urahisi.

### 3.4 Kundi Lengwa

Kundi lengwa ni jumla ya watu au vitu vyote ambavyo mtafiti amevikusudia na ambao/ambavyo kutoka kwao atapata taarifa anazozihitaji katika utafiti wake (Kombo na Tromp 2006; Enon 1998). Kwa hiyo, walengwa wa utafiti huu ni tamthilia za Emmanuel Mbogo za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora* Mtafiti aliziteua tamthilia hizo kwa kuamini kuwa mtunzi ametumia mitindo ya korasi. Kwa mnasaba huu, mtafiti aliamini kuwa kazi hizo zilikuwa na matumizi ya korasi zilizobeba dhamira za mtunzi.

### 3.5 Sampuli

Sampuli ni istilahi inayotumika kwa maana ya sehemu ya watu au vitu vinavyotafitiwa kutoka katika kundi kubwa. Sehemu hiyo huteuliwa na mtafiti kwa

kuzingatia sifa na tabia zao ambazo zinaweza kukidhi katika kuwakilisha kundi kubwa la watu waliobakia ili hatimae kujibu maswali ya utafiti (Kothari, 1999). Hivyo, utafiti huu ulitathmini mbinu za kikorasi na namna vinavyoibua dhamira kwa muktadha wa kiulinganishi katika tamthilia za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane* na *Samora*. Kazi hizo ndizo sampuli ya utafiti huu na zilichaguliwa kutokana na upya/usasa mkubwa uliomo miongoni mwa wasomaji wa kazi za Fasihi ya Kiswahili.

## 3.6 Usampulishaji

Enon (1999) anaelezea kwamba uteuzi wa watafitiwa ni kitendo cha kuchagua au kupata kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa. Vile vile, usampulishaji huelezwa kuwa ni mchakato wa kuchagua watu au taasisi kutoka kundi kubwa la watu ambalo litawakilisha kundi kubwa wakati wa kufanyiwa utafiti. Hivyo, katika utafti huu mtafiti alitumia usampulishaji lengwa. Kwa mujibu wa Enon (kashatajwa) uteuziwa sampuli lengwa ni ule wa mtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data anazozihitaji ili kupata data za utafiti wake. Mtafiti alizichagua kazi teuliwa kwa sababu aliona hazijafanyiwa utafiti kwa kutumia nadharia ya Korasi na Nadharia ya Fasihi Linganishi katika kiwango cha uzamivu. Hivyo, mtafiti aliamini kuwa, kazi hizo zitatoa picha ya uhalisia wa kile kinachotafitiwa. Aidha, kazi hizo ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa kwa sababu mtafiti aliamini kuwa kazi hizo zina matumizi ya korasi miongoni mwa fasihi ya Kiswahili.

### 3.6.1 Usampulishaji Lengwa

Babbie (1999) anaeleza kuwa usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa

sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza malengo ya utafiti wake. Hivyo, mtafiti aliteua kazi teule kwa kutumia mbinu hii. Tulitumia mbinu hii kwa sababu sampuli lengwa ina manufaa makubwa kwa mtafiti kwani humwezesha kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi. Hii ni kwa sababu mtafiti hatumii muda mwingi kwenda kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiki bali huegemea kwa watafitiwa watokanao na sampuli lengwa tu, ambapo mtafiti alipobaini maneno, sentensi au aya katika tamthilia teule inayohusiana na madhumuni yake ya utafiti basi aliyadondoa katika daftari hilo kama lilivyopangwa.

## 3.7 Data za Utafiti Zilizokusanywa

Katika utafiti wowote ule wa kitaaluma huwa kunakuwa na data za aina mbili. Data hizo ni za msingi na upili. Katika utafiti huu tulikusanya data za msingi na za upili ili kuweza kukamilisha madhumuni ya utafiti wetu.

### 3.7.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza (Furlong, 2000). Young (26.1984), katika Salim (2015) anasema kwamba data za msingi pia hujulikana kama data ghafi ambazo ndiyo kwanza zinaingia katika taaluma ya utafiti kwa mara ya kwanza tayari kwa ajili ya kuchambuliwa na kuchanganuliwa. Data hizo zikishachambuliwa na kuandikwa katika ripoti au tasnifu hubadilika jina na kuwa ni data za upili

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi (Kothari, 2004). Data hizi za msingi huwa hazijapata kukusanywa na mtafiti

mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama huu ambao unakusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza. Data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kutoka tamthilia za *Sadaka ya John Okello* na *Mondlane na Samora*.

### 3.7.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu, tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeo katika maktaba mbalimbali (Creswell, 2009). Aidha, data za upili hupatikana kwa kupitia maandiko kama vile ripoti za miradi, hotuba za viongozi ambapo mtafiti hupata data na kuzitumia katika utafiti wake.

Salim (2015) anasema kuwa lengo kuu la kukusanya data za upili ni kwa ajili ya kujazilishia na kukazia maarifa yanayotolewa kupitia data za msingi. Data za upili hukusanywa na mtafiti ili kuchagua machapisho ambayo yanaendana na mada yake ya utafiti kisha kuyasoma machapisho hayo kwa kina kwa lengo la kupata data za upili. Data hizo hutumika wakati wa uchambuzi wa data za utafiti kwa kurejelewa hapa na pale ili kushadadia hoja za data za msingi.

Kothari (2004) anaeleza kwamba data za upili ni data ambazo zimekwisha kusanywa na watafiti wengine na kuchapwa ama kuandikwa. Hii ni kusema kwamba data za upili huwa tayari zimewahi kufanyiwa utafiti. Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za upili kutoka katika machapisho mbali mbali ya waandishi. Data hizi zilimsaidia mtafiti kuthibitisha data za msingi na hivyo kufikia lengo la utafiti. Hivyo, ili kuzipata data hizo mtafiti alisoma machapisho mbali mbali katika maktaba

za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Maktaba Kuu ya Taifa tawi la Pemba.

## 3.8 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (2008) anaeleza kuwa dhana ya ukusanyaji wa data kuwa ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kufanikisha lengo lake la utafiti. Pia, mbinu za kukusanya data huweza kufafanuliwa kama njia zinazotumika katika kufanikisha zoezi la kukusanya data za utafiti. Hivyo, utafiti huu ulikusanya data zake kwa kutumia mbinu za upitiaji wa nyaraka maktabani na usomaji makini wa tamthilia teule. Mbinu ya upitiaji wa nyaraka ilitumika katika kukusanya data za upili na mbinu ya usomaji makini ilitumika katika kukusanya data za msingi.

### 3.8.1 Usomaji Makini

Usomaji makini au wakati mwingine hujulikana kama usomaji wa kina ni mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka katika matini zilizoteuliwa katika utafiti husika (Kothari, 2008). Kupitia mbinu hii, mtafiti huteua matini maalumu na kuzisoma matini hizo kwa kina huku akidondoa baadhi ya maneno, sentensi au aya ambazo ndizo huwa data za utafiti wake.

Data za msingi katika utafiti wetu ndizo zilikazokusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kutoka katika tamthilia teule. Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti aliandaa daftari maalumu alililoligawanya sehemu kuu tatu na kila sehemu ikiwa na kichwa cha habari kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Hii ilirahisisha zoezi la ukusanyaji wa data.

### 3.8.2 Upitiaji wa Nyaraka

Neno “nyaraka” linarejelea machapisho na maandiko mbali mbali yanayopatikana katika maktaba. Kimsingi, mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti, kukusanya machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa uzingativu (Kothari, 2008). Aidha, Salim (2015) anamnukuu Merrian (1998), akieleza kuwa katika maktaba mtafiti huweza kupata data nyingi, kwa urahisi bila gharama. Data za upili pamoja na kutumika katika kushadadia hoja zitokanazo na data za msingi katika uchambuzi wa data lakini pia hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasnifu inayohusika na “Mapitio ya kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia”. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kituo cha Pemba, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Maktaba ya Chuo Kikuu Chukwani. Katika maktaba hizi mtafiti alisoma makala, ripoti, tasnifu, majarida, vitabu na maandishi pepe katika wavuti na tovuti zilizohusiana na mada ya utafiti wake.

## 3.9 Mkabala wa Uchambuzi wa Data za Utafiti

Uchambuzi wa data ni kitendo muhimu sana katika kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanapatikana na hivyo utafiti mzima nao kukamilika. Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo na kitakwimu kuchambua na kujadili data za utafiti na matokeo yake. Kothari (1990) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Mbinu ya kimaelezo hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi kwa sababu fasihi ni

taaluma ya maneno aidha ya kuandikwa au kuzungumzwa. Mbinu hii ilitumika ili kuchambua data tulizozikusanya kwa usomaji makini. Hivyo, mtafiti aliona mbinu hii ya uchambuzi wa data ilikuwa rahisi kufikia malengo ya utafiti huu.

## 3.10 Zana za Kukusanyia Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia dhana zifuatazo:

### 3.10.1 Shajara

Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2013), shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku. Zana hii ilitumika kuhifadhi kumbukumbu za data zilizopatikana katika utafiti huu. Kwa kutumia zana hii, mtafiti aliandika katika shajara taarifa mbalimbali zilizonukuliwa kutoka katika tamthiliya teule.

### 3.10.2 Kompyuta

Kompyuta ni zana ambayo mtafiti aliitumia tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake. Komyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazoingizwa ndani yake (BAKIZA, 2010). Mtafiti aliitumia zana hii kuchapa kazi yake ya utafiti, kuhifadhi data, kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali yahusuyo utafiti huu yanayopatikana katika tovuti na wavuti mbalimbali.

## 3.11 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

### 3.11.1 Usahihi wa Data

Usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika za utafiti (Cohen na wenzake, 2000). Usahihi wa data katika utafiti huu ulihakikishwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na upitiaji wa

nyaraka. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kimaelezo na wa kitakwimu ndio uliotumika. Vile vile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake.

### 3.11.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale ya utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Kothari, 2008). Kuaminika kwa data kunajitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano ama ulingano katika taarifa zinazotolewa na watu wale wale kwa muda tafauti (Furlong na Lavelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikishwa kwa kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Korasi na mbinu nyengine mchanganyiko za kukusanyia data.

### 3.11.3 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti huhusishwa na mila na desturi ambayo jamii huyaamini katika eneo ambalo mtafiti analenga kuchunguza kitu au jambo fulani. Lengo la maadili katika utafiti ni kulinda mambo ya kibinaadamu yanayoaminiwa na jamii. Pia, kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika katika muktadha unaokubalika; kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu au jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa miradi ya kitafiti inazingatia maadili, kama vile; masuala ya uongozi na athari zake, utunzaji siri na utoaji wa habari (http://researchethics). Salim (2015) anasema miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa mtafiti kuvizingatia ni maadili ya utafiti yanayohusu

ERROR: syntaxerror
OFFENDING COMMAND: --nostringval--

STACK: